# HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

SHULE YA SEKONDARI NGONGO,

S.L.P 383,

LINDI.

TAREHE ......................

**MWANAFUNZI.........................................................**

## YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA I MWAKA 2021**

## SHULE YA SEKONDARI NGONGO

1.0 Ninapenda kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ngongo kwa mwaka wa masomo **2021**. shule ya sekondari ngongo ni ya kutwa yenye mchanganyiko wa wasichana na wavulana kwa kuchangia gharama ya chakula .shule inapatikana katika mkoa wa **LINDI** ,Manispaa ya **LINDI** ,Kata ya jamhuri , mtaa wa kiduni , eneo la tulieni , jirani kabisa na viwanja vya maonesho ya nanenane kanda ya kusini Ngongo . Shule ipo umbali wa kilomita 15 kutoka makao makuu mkoa na wilaya katika barabara iendayo mkoani lindi . Nauli ya basi kutoka kituo cha mabasi lindi mjini hadi shuleni ni Tshs 1000/=.
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 06/01/2020.unatakiwa kuripoti shule tarehe 06/01/2020 bila kuchelewa na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2020 . Baada ya tarehe hiyo msako wa wanafunzi ambao hawajaripoti utafanyika na mzazi ambaye hatamleta mtoto wake shule atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ikiwa ni kulipa faini au kifungo au vyote kwa pamoja .

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NGONGO**

**..............................................**

**ALPHONCE A. NGAJIRO**

**MKUU WA SHULE**

**SIMU: 0714124217/0625773052**

## 2.0 MAHITAJI MUHIMU SHULENI

### 2.1 SARE ZA SHULE

#### 2.1.1 WAVULANA

**(a)** Suruali mbili(2)rangi ya damu ya mzee mshono wa kawaida wenye marinda mawili kila upande na pindo la chini.
(b) Mashati mawili (2)meupe ya mkono mifupi
(c)Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi , vya kaba visivyo na madoido au visigino virefu
(d)Soksi nyeupe jozi zakutosha zisizo na urembo wa aina yoyote
(e)Fulana mbili 2) za njano zisizo na maandishi yoyote zitatumika wakati wa masomo ya jioni na kazi za jioni .
(f)Fulana yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni kwa tsh 15000/=itakayotumika siku ya jumatano na wakati wa masomo ya jioni na kazi
(g) Suruali mbili(2)za light blue mshonono wa kawaida wenye marinda mawili kila upande na pindo chini zitakazovaliwa wakati wa kazi za jioni au masomo ya jioni
(h)Sweta rangi ya damu ya mzee litakalovaliwa nyakati za baridi.
(i)nembo ya shule inapatikana shuleni
(j)Tai mbili (2)ndefu rangi ya damu ya mzee.
(k)Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi
.

#### 2.1.**2 WASICHANA**

(a) Sketi mbili (2) ndefu za heshima rangi damu ya mzee zenye malinda ya kawaida.
(b) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi / nusu kanzu za tetroni na hijjab yake ndefu kwa watakaovaa hijjab .
(c) Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi , vya kamba visivyo na madoido wala visigino virefu.
(d) Soksi nyeupe jozi za kutosha zisizo na urembo wa aina yoyote .
(e) Fulanambili (2) moja ya njano isiyo na maandishi yoyote, nyingine ni yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni kwa Tshs 15,000/= zitakazotumika wakati wa masomo ya jioni .
(f) Magauni mawili marefu ya light blue mshono wa solo yakayovaliwa wakati wa kazi za jioni au masomo ya jioni.(kwa wanaovaa hijjab washone na hijjaab yake )
(g) sweta rangi ya damu ya mzee litakalovaliwa nyakati za baridi.
(h) Nemboya shule inapatikana shuleni
(i) Tai mbili (2) ndefu rangi ya damu ya mzee .

<u>ZINGATIO:</u> **VIMODO NA KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI HATURUHUSU, TUTAZICHANA!!! .**

**1.1 SARE ZA MICHEZO.**

- Fulana na bukta ya rangi ya bluu kwa wavulana.
- Traki suti ya pink au light blue kwa wasichana .
- Raba au viatu vyovyote vya michezo kwa wasichana na wavulana .

**2.3: VIFAA VYA USAFI**

**2.3.1 KWA WAVULANA**

- Jembe ngwamba 1 lenye mpini .
- Panga 1
- Fyekeo 1
- Fagio laini 1 la plastiki.
- Ndoo 1 ndogo

**2.3.2 KWA WASICHANA**

- Jembe ngwamba 1 lenye mpini .
- Panga 1
- Fyekeo 1
- Fagio wa mti wa chelewa 1
- Ndoo 1 ndogo

**2.4 VIFAA VYA DARASANI.**

(a) Madaftari makubwa 15 (counter book)quire 2/3,rula 1 ndefu na mkebe 1(mathematical sets)
(b) Kamusi ya kiingereza /kiingereza – LAZIMA
(c) Begi lakuhifadhia madaftari
(d) Faili ( box faili au plastiki )
(e) Peni na kalamu za risasi za kutosha .

**2.5 MAAGIZO MENGINE YA KUZINGATIA**

(a) Cheti cha uthibitisho kutoka kwa daktari ili kufahhamu mwanafunzi ana maradhi yatakayo hitaji uangalizi maalumu
(b) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
(d) Picha au paspoti za mzazi au mlezi ambaye atatambulika shuleni endapo atahitajika

## 2.6: MAHITAJI KWA WATAKAO KAA HOSTELI
### 2.6.1 CHAKULA NA WAPISHI.

- Pesa ya chakula nakulipa wapishi kwa mwaka ni **Tshs 360,000/=(**Ilipwe kwaawamu moja au mbili)
  **ZINGATIO** : Fedha za CHAKULA NA WAPISHI zilipwe akaunti ya shule **70201601426**.NMB. Jina la akaunti **ni NGONGO SECONDARY SAVING ACCOUNT**. HATUPOKEI PESA TASLIMU MKONONI

2.6.2 VIFAA VINAVYOHITAJIKA HOSTELI

a) Godoro 1 la futi 2.5x6
b) Mto 1 na foronya rangi ya shuka
c) Shuka 2 za light blue au pink.
d) Kadi ya bima ya afya . (LAZIMA )( Kwa wasio kuwa nayo wataunganishwa na CHF kwa gharama zao wenyewe )
e) Chandarua 1( neti ya mbu) rangi ya blue
f) Pasi 1 ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo
g) Ndala /yeboyebo ya kuogea
h) Ndoo za maji kwa matumizi binafsi
i) Taa ya sola kwa matumizi binafsi ya dharura
j) Dumu la lita 5 kwa ajili ya kuhifaa dhia maji ya kunywa .
k) Sahani,bakuli,kikombe na kijiko vya bati kwa ajili ya chakula
l) Sabuni za kuogea na kufulia , taulo , dawa za meno,mafuta ya kupaka na pedi za kutosha kwa wasichana .
m) Fedha kwa matumizi madogomadogo ,na matibabu na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo

**SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na elimu nchini .hivyo mwanafunzi anapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara kwa mara na walimu wakati wote awapo shuleni :

(a) Heshima kwa viongozi , wazazi,wafanyakazi wote , wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima .
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasani ni muhimu
(c) Kutimiza kwa umakini maandalio ya kujisomea jioni
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwapo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi katika shule hii
(f) Kutunza usafi wa mwili na usafi wa shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo ndani na nje ya shule
(h) Kuzingatia ratiba zote za shule wakati wote
(i) Lugha chafu , matusi,ugomvi,fitina kupigana ni mwiko kabisa .
(j) Unywaji wa vileo , kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote kwa mwanafunzi ni mwiko.
(k) Wizi wa aina yoyote ni marufuku kwa mwanafunzi.
(l) Uharibifu au upotevu wa mali za umma ni kosa kabisa.
(m) Wageni wa wanafunzi wataruhusiwa kuonana nao baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu . na ikumbukwe kwamba siku za kutembelea wanafunzi ni siku ya jumapili ya mwisho wa mwezi.
(n) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa /kuolewa . akibainika atafukuzwa shule mara moja , aidha ni marufuku kwa wanafunzi kuwa na mahusiano ya kimapenzi wakati wote akibainika adhabu yake ni kufukuzwa shule.
(o) Ni mwiko kwa mwanafunzi yeyote kwenda nyumba za walimu , wafanyakazi na mabweni ya jinsia tofauti bila ruhusa kutoka kwa walimu husika .
(p) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi , CD,Memory card au laini yoyote ya simu.
(q) Kukataa adhabu ni kukataa malezi bora ya walezi wako wa shule
(r) Kuchochea au kufanya mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku .
(s) Mwanafunzi anatakiwa kufuata maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

(t) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani.
(u) Ni marufuku kuvaa mavazi yasiyoruhusiwa shuleni
(v) Ni marufuku kwa mwanafunzi kujipikia chakula cha aina yoyote shuleni.
(w) Ni marufuku kwa mwanafunzi na wazazi kutumia simu za wapishi au walinzi kuwasiliana kwa namna yoyote ile .Mawasiano yote yafanyike kwa walimu na sio vinginevyo.

3.1 **MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA HIVYO JIEPUSHE NAYO.**

i. Wizi
ii. Uasherati ,na mahusiano ya kimapenzi ,usagaji, ushoga na ubakaji.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa kulevya kama vile bangi,milungi,kubelina cocaine.
iv. Kupiga au kupigana
v. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vi. Kudharau kwa bendera na wimbo wa taifa .
vii. Kuoan au kuolewa.
viii. Kugoma,kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama ndani na nje ya shule.
ix. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
x. Kumiliki simu ya mkononi shuleni .
xi. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina.
xii. Kunyanyapaa na uonevu wa aina yoyote.
xiii. Kuweka au kusababisha mimba ,kupata mimba /kuharibumimba kwa makusudi.
xiv. Kutoa kashfa au lugha ya matusi.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**SHULE YA SEKONDARI NGONGO**
**S.L.P 383**
**LINDI.**
**TAREHE………………….**

**MGANGA MFAWIDHI…………………………………………..**

**YAH: MWANAFUNZI …………………………………………………**

Amechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Ngongo mwezi januari 2020.kiutaratibu kabla ya kukubaliwa kuingia katika shule hii na kuendelea na masomo ni lazima apimwe afya kwanza , ili itusaidie kutambua afya yake .

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika hapa chini baada ya kupimwa.

Ahsante kwa ushirikiano

**……………………………**

**VICTORIA G. HOKORORO**

Tafadhali onesha kama mwanafunzi mhusika amewahi au ana magonjwa yafuatayo kwa kuweka alama V sehamu inayohusika.

1. Kifafa(Epilepsy) Ndio…………..Hapana …………….
2. Moyo (heart disease) Ndio…………..Hapana ……………
3. Magonjwa ya akili(mental case) Ndio…………..Hapana ……………
4. Ukosefu wa damu( anemia siclecell Ndio…………..Hapana ……………
5. Kifua kikuu(T.B) Ndio…………..Hapana ……………
6. Pumu (asthmatic case) Ndio…………..Hapana ……………
7. Kisukari Ndio…………..Hapana ……………
8. Kichocho (Bilharzias) Ndio…………..Hapana ……………
9. Malaria sugu(chronic malaria) Ndio…………..Hapana ……………
10. Magonjwa ya zinaa (vernadal disease) Ndio…………..Hapana ……………
11. Je ? ana dosari nyingine yoyote ya kiafya? Ndio…………..Hapana ……………
12. ujauzito Ndio…………..Hapana ……………
13. macho Ndio…………..Hapana…………….

**JINA LA MGANGA……………………………………..**

**SAHIHI…………………………………………..**

**TAREHE…………………………………………**

**MUHURI…………………………………………..**

## TAARIFA MAALUMU YA KUHUSU MWANAFUNZI

**SEHEMU A( IJAZWE KWA HERUFI KUBWA)**

**Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………………………**
**Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………….**
**Anwani ya nyumbani ……………………………………………………………….**
**Namba ya simu ………………………………………………………………………**
**Kata……………………..jina la mtendaji kata……………………………………namba simu………………… sahihi/muhuri…………………………….**
**Mtaa……………………,Jina la mtendaji wa mtaa……………………………………. Namba ya simu…………………………….. sahihi / muhuri……………………………………….**

**SEHEMU B**

**Jina la Baba/mlezi…………………………………….hai /amefariki.**

**Kazi ya Baba / mlezi………………………………Namba ya simu………………………..**

**Jina mama/mlezi…………………………………hai/amefariki.**

**Kazi ya mama/mlezi…………………………..namba ya simu………………………..**

**SEHEMU C TAARIFA ZA NDUGU WA KARIBU**

| JINA NDUGU | UHUSIANO | KIWANGO CHA ELIMU | ANWANI/NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**SEHEMU D:MICHEZO /SANAA ANAYOPENDA**

| JINA LA MCHEZO | SHULE | TOKA MWAKA | HADI MWAKA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

**SEHEMU E:KAZI/UONGOZIALIYOWAHI KUFANYA**

| KAZI/CHEO | SHULE | TOKA MWAKA | HADIN MWAKA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

1. **Ninahaidi kuwa na tabia nzuri mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.**
2. **Nitafuata taratibu na sheria nitakazoelekezwa nitakapoenda kinyume sheria ichukue mkondo wake.**
3. **Utoro kwangu ni mwiko**
   **Sahihi ya mwnafunzi…………………………………………**
   **Sahihi ya mzazi……………………………………………**
   **Tarehe ……………………………………………………**

**AHADI YA MZAZI KUKUBALI MWANAYE KUJIUNGA NA SHULE**

**Mimi …………………………………………………mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………………………. Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Ngongo , kidato cha kwanza mwaka 2020.**

i. **Nakubali /sikubali mwanangu kusoma katika shule hii.**
ii. **Ninaahidi nitatii/sitatii na kumuimiza mwanangu kutii/kutotii sheria zote kwa mujibu wa kanuni na taratibu kama nilivyofahamishwa na uongozi wa shule.**
iii. **Nakubali/sikubali mwanangu kuadhibiwa kwa mujibu na taratibu endapo atavunja au kukiuka taratibu zza shule.**
iv. **Wakati wote mwanangu atakapokuwa shuleni (mwanafunzi)hana ruhusan kwenda kwenye nyumba za wageni ,maeneo ya ulevi kumbi za semina na muziki.**
v. **Ninaahidi kumpatia vifaa vyotevinavyohitajika kwa wakati.**
vi. **Ninaahidi kumleta shuleni kwa wakati bila kuchelewa.**
vii. **Ninaahidi kushirikiana na walimu katika kufuatilia maendeleo ya watoto kitaaluma .**
viii. **Ninaahidi nitahudhuria vikao vyote pindi vitakavyohitajika.**

**KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI**

**Jina la mwanafunzi……………………………………………………………………………..**

**Tarehe yakuzaliwa……………………………………………………………………………….**

**Mimi……………………………………………………………………………………………………………**

- **Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali kuwa serikali ya Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo,ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi kwa nafasi yangu katika kuleta maendeleo yake.**
- **Hivyo ninaahidi kwamba nitajibiidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule ili kutimiza shabaha hiyo ,ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe na nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa na iwapo nitakiuka sheria za shule niadhibiwe kulinga na sheria na kanuni zinavyosema.**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI………………………………………….. TAREHE…………………………………….**

**B. SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI**

**Mimi……………………………………………………………………………………………………**

**Ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi tajwa hapo juu ,naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu.**

**Nitakuwa tayari kushirikina na uongozi w shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nipo tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewiwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.**

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI………………………………………………………………….**

**TAREHE……………………………………………………………………………………..**